

**MAADILI>>Kila familia ina wajibu w**

**UHURU**

MAONI YA MHARIRI

## Watumishi wazingatie agizo la Simbachawene

WATUMISHI katika Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Umma, hawana budi kujitathmini, kuhusu ushauri uliotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene.

Waziri huyo aliwataka watumishi hao kwenda kwa wananchi kusikiliza malalamiko yao na kuyatafutia ufumbuzi kwa dhumuni la kuondoa matatizo ndani ya jamii

Simbachawene alisema hayo jijini Arusha, juzi, alipofungua kikao kazi cha Wachunguzi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Watumishi hao hawana budi kutambua kazi wanayoifanya ni kuwatumikia Watanzania, hivyo wanawajibika kuwafuata wananchi walipo kujua changamoto zao.

Tunaunga mkono ushauri wa Waziri Simbachawene wa kutaka watumishi kuwafuata wananchi kujua changamoto zinazowakabili, badala ya kukaa ofisini kusubiri wachache wanaolalamikia viongozi.

Watumishi wanapaswa kutambua baadhi ya wananchi hawafiki ofisini kueleza changamoto zao kutokana na sababu mbalimbali, hivyo wakati umefika kwa kuwatembelea na kuwapa nafasi ya kueleza yanayowasibu.

Hakika watumishi wakifanya kazi yao kwa kuzingatia weledi na kukukumbuka viapo vyao vya kuwahudumia wananchi, hatua hiyo itasaidia kupunguza matatizo yaliyopo miongoni mwa jamii.

Kelele za wananchi zinaposikika ni vema zikawakuta huko huko viongozi walipo, itasaidia kutatua kero zao na kuwafanya viongozi kujirudi na kufuata misingi ya maadili katika utendaji kazi.

Tunampongeza Waziri Simbachawene kuwakumbusha viongozi kufuata sheria, taratibu na kanuni katika utumishi wa umma kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kuwahudumia wananchi.

Wananchi wanapokosa huduma katika chombo kinachopaswa kuwahudumia na badala yake wanaishia kulalamika ni aibu kwa taasisi husika na nchi kwa kwa ujumla.

Kila kiongozi anapaswa kutimiza wajibu wake kwa kufanya kazi kwa bidii kubwa kusaidia kuondoa malalamika ndani ya jamii ambayo kila kukicha yanakuwa na kuleta adha kubwa kwa jamii.

Kuwajibika kwa kila kiongozi kutasaidia kuondoa kelele kwa jamii na kila mmoja atakuwa ametimiza jukumu la kusimamia maadili ndani ya jamii.

Ikumbukwe kuwa wananchi wana changamoto nyingi, ambazo asilimia kubwa zimefanyiwa kazi na kilichobaki ni kwa viongozi kuwa mstari wa mbele kutatua shida zao kwa haraka mkubwa.

Hivyo, tunatumaini makubwa agizo la Waziri Simbachawene litafanyiwa kazi kwa kila kiongozi kusimama imara kwa kubadilika na kufanya kazi kwa bidii kuondoa matatizo ndani ya jamii.

### Uhuru Publications Limited (UPL)

S.L.P. 9221, Dar es Salaam

Makao Mkuu: Mtaa wa Lumumba Mkabala na Shule ya Msingi Mnazi Mmoja

Chumba cha Habari:

+255-739 957 882/FAX: 2183780

email: uhurunews@yahoo.com

uhuruadvert@gmail.com

uhurumakala@gmail.com

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu: \_\_\_\_\_ 0655 - 355810

Naibu Mhariri Mtendaji: \_\_\_\_\_ 0784 - 599717

Mhariri wa Habari: \_\_\_\_\_ 0713 - 117177

Mhariri wa Makala: \_\_\_\_\_ 0754 - 305135